# Leo hii Maandiko Haya Yametimizwa

Jeffersonville, Indiana, USA

Februari 19, 1965

1 Endeleeni tu kusimama, mkipenda, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa maombi.

Mpendwa Baba wa Mbinguni, tunashukuru usiku wa leo kwa ajili ya hii, nafasi nyingine ya kuja na kuwasilisha Injili hii tukufu, ya ajabu ya Yesu Kristo. Tunakushukuru kwa sababu Yeye angali ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tunakushukuru kwa ajili ya watu hawa ambao wamekusanyika hapa nje katika wakati huu wa hali ya hewa ya baridi, na wangali na matarajio yao makubwa, wakitazama, wakiamini ya kwamba tutapewa kitu kisicho cha kawaida kutoka kwa Mungu. Tunakuja na tumaini hilo, Bwana, kwa kila mkutano. Twakushukuru kwa ajili ya ibada za juzi usiku maskanini. Twakushukuru kwa ajili ya ibada hapa jioni iliyopita na kwa ajili ya ibada ya leo maskanini. Tunatazamia sasa kile utakachokuwa nacho kwa ajili yetu usiku wa leo.

Baba, tunajua ya kwamba mtu ye yote anayeweza kusogeza mikono yake angeweza kufungua kurasa za Biblia, bali kuna Mmoja tu anayeweza kuifanya hai na kuwa halisi, na huyo ni Wewe. Na, Baba, tunakutazamia kufanya jambo hilo usiku wa leo. Tubariki katika kila njia. Mioyo yetu imejaa furaha sana tunapoona wakati ukikaribia ambapo tutakutana Naye, uso kwa uso, Yeye ambaye tumempenda na kuishi kwa miaka hii yote.

Waongofu wapya wengi, Bwana, wameletwa. Tukifahamu ya kwamba jeshi kubwa, arobaini ama hamsini, litabatizwa katika Jina Lako, asubuhi, kutoka kwenye ibada jana usiku. Ee Mungu, tafadhali endelea, tunaomba, mpaka kila Mzao wa Mungu aliyechaguliwa tangu asili ameiona Nuru ya Injili, na ameingia zizini.

Tunakuomba utufiche usiku wa leo nyuma ya Neno; tupofushe na mambo ya ulimwengu, na hebu tumwone Yesu. Jalia kuwe na tukio la Mlima wa Kugeuzwa Sura miongoni mwetu, usiku wa leo, tusimwone mtu ye yote ila Yesu peke yake. Tunaomba katika Jina Lake, na kwa ajili ya utukufu Wake na thibitisho la Injili Yake. Amina.

Mnaweza kuketi.

2 Nitageuza tu maikrofoni hii, ama dawati hili, upande kidogo tu, kama ni sawa, kusudi niweze kuona pande zote mbili za wasikilizaji. Nadhani ninaweza kupata maikrofoni hizi hapa vizuri. Vema, hebu kidogo.

Tunatoa salamu, kutoka kwenye jumba kuu la mikutano hapa usiku wa leo, marafiki zetu huko Arizona, California, Texas, na kote Marekani, kwa njia ya simu. Hii, hii inaendelea kote nchini, ibada hii usiku wa leo, kwa njia ya simu, kwa hiyo tunatumaini ya kwamba Mungu atatubariki.

Mnaweza kusikia, huko nyuma kwenye—kwenye ukumbi upande wa kushoto? Vema, wataangalia sasa mfumo wa simu, kuona kama unafanya kazi vizuri.

3 Kila mtu ana furaha usiku wa leo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Aisee, hilo ni sawa! Upande huu? ["Amina."] Amina. Nina furaha sana kuona ya kwamba ninyi nyote mmeketi vizuri.

Na sasa kesho usiku, kama umati ukiendelea kuongezeka, wao pia watakuwa wa moja kwa moja kwa simu. Kuna usiku wa leo. Nafikiri baadhi yao wako huko maskanini.

Na, kesho asubuhi, ibada haziwezi kufanywa maskanini, kwa sababu … kutakuwa na mtaalamu wa maua pale atakayelipamba kanisa kwa ajili ya arusi kesho alasiri. Nao wamehamisha zile—zile ibada, asubuhi, hadi kwenye kanisa la Ndugu Ruddell, mmoja wa washirika wetu, na huko juu kwenye—kwenye barabara kuu hapa, 62. Imetangazwa? [Ndugu Neville anasema, "Naam." — Mh.] Imetangazwa. Na, kama ikifurika kule juu, tutachukua waliosalia na kumtuma mhudumu mwingine kwa Ndugu Junior Jackson, huko Clarksville. Kusudi la kuifanyia kwa Ndugu Ruddle, ni karibu na hapa nasi twaweza—nasi tulidhani mngepapata hapo kwa urahisi. Na ndipo tutalishughulikia kwa njia fulani. Hakikisha ya kwamba wale wote watakaobatizwa wamefika kesho, nami natumai kutakuwako na wengine mia moja au mbili watakaoongezeka kwa wale watakaobatizwa kesho. Na sasa kesho usiku …

4 Sipendi kutangaza cho chote utakachonena mbele ya wakati huo, lakini usiku mmoja katika ibada au siku moja, ninataka nihubiri kuhusu Je, *Huyu Melkisedeki Ni Nani?* Kwa kuwa ni—ni somo ambalo nadhani tunaishi katika wakati huo ambapo mafunuo hayai yamekuwa swali katika nyakati zote juu ya, "Je, Mtu huyu ni nani?" Nami ninaamini ya kwamba Mungu ana jibu, kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Wengine walisema, "ukuhani," wengine walisema, "mfalme," wengine … Lakini kuna ninii …

Mradi tu kuna swali, hapana budi kuwe na jibu kwa swali hilo, ambalo ni kweli. Hakuwezi kuwa na swali bila kwanza kuwapo jibu.

5 Sasa, tunatumaini ya kwamba Mungu atatupa baraka usiku wa leo kutoka kwenye Neno Lake, tunapolisoma.

Nawe umekuwa na … Billy aliniambia niwaambie ya kwamba hakika mmekuwa na ushirikiano mzuri na watu hapa ambao wamekuwa kwenye mfumo wa maegesho, polisi na kila kitu. Endeleeni; hilo ni zuri sana.

Twatumai kuona wakati, labda hivi karibuni, ambapo tungeleta hema hapa mjini na kulipiga hapa katika kiwanja cha mpira ambapo tungekaa kwa wakati mrefu zaidi, labda kwa mkutano wa majuma matatu au manne, mfululizo. Na hapa tunafahamiana kwa shida, na halafu hatuna budi kuaga na kwenda tena. Lakini ningependa kuja na kukaa safari ndefu, wakati mmoja ambapo mngeweza kukaa kwa hiyo haitubidi kufunga kwa usiku mmoja ama miwili, bali tukae tu na kufundisha, mchana na usiku, mchana na usiku, kuendelea na kuwasha. Labda mtu fulani aende nyumbani na kulisha kuku kukama ng'ombe, na kurudi juma lifuatalo na kuendelea na ibada. Ni—ninapenda jambo hilo. Kwa hiyo Bwana awe pamoja nanyi.

6 Sasa, kabla sijaondoka, labda Jumapili asubuhi au Jumapili usiku, ama wakati fulani, moja ya ibada hizi, ninajua nyote mnangojea kusikia Ujumbe juu ya Kweli kuhusu *Ndoa Na Talaka*, ambayo ni moja ya matatizo makubwa ya siku hizi. . Nami nina hakika tu kama ninavyosimama hapa, ninaamini ya kwamba jibu sahihi liko katika Neno la Mungu, nami ninaamini hilo ndilo nililoahidi kurudi kwa ajili yake.

Nami nadhani, kwa kujua, kadiri nijuavyo, ninataka kuwa na ibada nyingine hapa Jeffersonville, Jumapili ya Pasaka, nasi tutaninii … kwa ajili ya ibada ya kuchomoza kwa jua, na halafu Jumapili ya Pasaka. Kwa hiyo tutalitangaza mbele na kujaribu labda kupata ukumbi, ikiwezekana, ama mahali fulani, kwa ajili ya Jumapili, labda tuje Jumamosi na Jumapili. Inanibidi kuruka na kurudi, kwa sababu wakati umekaribia … Sina budi kuyachunguza, kwanza, kwa ratiba niliyo nayo, na moja ya ratiba ya—ya—yangu huko California. Halafu basi, mara baada ya jambo hilo, sina budi kushuka kwenda—kule Afrika. Kwa hivyo kuweni karibu na mniombee.

7 Sasa, usiku wa leo, ninataka kuwaelekeza kwenye sehemu ya Neno la Mungu, inayopatikana katika sura ya 4 ya Luka Mtakatifu. Mlango wa 4 na kifungu cha 16, utaanza, Yesu akinena.

> *… Leo hii Neno hili limetimizwa masikioni mwenu.*

Sasa tunataka kupata, kutoka Kwake, hitimisho la jinsi Neno la Mungu lilivyo na nguvu! Sasa, sisi sote tunaweza kujua mitambo, bali inahitaji Nguvu za Utendaji kuifanya ifanye kazi.

Tunaweza kujua ni nini mitambo ya mashine, motokaa, lakini basi inachukua nguvu za kufanya magurudumu kuanza kufanya kazi na kusonga mbele.

Sasa, Yesu alikuwa amerudi Nazareti, ambako alilelewa. Huko chini katika Maandiko hapa, tunaona ya kwamba walisema, "Tulisikia ulifanya *hivi na vile* huko Kapernaumu. Sasa hebu tuone Wewe ukifanya jambo hilo hapa katika nchi Yako Mwenyewe."

Yesu alisema, "M—nabii hakosi heshima ila katika nchi yake." Na, bila shaka, hapo ndipo ulipolelewa, na ambapo watu wanakujua. Na pale Yeye alikuwa na jina ba—-ba—-baya kwanza kwa kuzaliwa bila baba wa kidunia. Wao walimwita "mtoto haramu," ya kwamba Mariamu kweli alikuwa na mimba kabla hajaolewa, rasmi, Yusufu. Lakini, hilo sivyo, tunajua sivyo ilivyo.

8 Na, juu ya Andiko hili, kile kilichosababisha mimi, kulitazama, kilikuwa kitu fulani kilichotendeka hivi majuzi huko Phoenix, Arizona. Ilikuwa ni siku ya mwisho, ya ibada niliyopaswa kuhubiri kwenye Mkutano wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Injili Yote.

Na katika mkutano huu kulikuweko mgeni pamoja nasi aliyekuwa askofu wa Kikatoliki, ambaye yeye yu wa Ushirika wa Kikaldayo wa Kanisa Katoliki la Kimitume—Padre Mkuu John S. Stanley, O.S.D. Yeye ni Askofu mkuu wa maaskofu wa Nchi ya Amerika katika Kanisa Katoliki. Hii ilitokea kuwa kadi yake na—na anwani yake.

Naye alikuwa mgeni pamoja na Wafanyi Biashara Wakristo, nami nilikuwa nimemwona pale, siku iliyotangulia. Na nilipokuwa nikizungumza Jumamosi usiku, naamini ilikuwa, ama Jumamosi asubuhi kwenye kiamshakinywa, nami … Nilipokuwa nikizungumza, yeye aliendelea kuniangalia. Nikawaza, "Mtu huyo hakika hakubaliani na kila kitu ninachosema." Na, unajua, ungeweza—ungeweza tu kumwona; angeweka kichwa chake juu-na-chini, lakini sikujua ni kitu gani hasa kilichokuwa kikitenda kazi ndani yake.

9 Kwa hiyo Jumapili alasiri, nilipoamka kuzungumza, nilikuwa nikienda kuchukua somo langu juu ya *Uchungu wa Kuzaa*, ambapo Yesu alisema, ya kwamba, "Kama mwanamke aliye katika utungu wa kuzaa," anatungu katika kuzaa. Na kwa hiyo nilikuwa nizungumze kutoka hapo, kama, *Utungu wa Kuzaa*, somo, nikisema ya kwamba ulimwengu uko katika utungu wa kuzaa sasa. Mambo ya kale hayana budi kuondolewa, ili yale mapya yapate kuzaliwa; kama tu vile mbegu inavyopaswa kuoza, kusudi ipate uhai mpya.

Na jinsi uchungu, utungu wa kuzaa ulivyoipiga dunia! Katika Vita vya Kwanza vya Dunia, alikuwa na

maumivu makali sana, kwa sababu walikuwa na gesi yenye sumu, na kadhalika, ambayo karibu ingeweza kuuangamiza ulimwengu. Na katika Vita vya Pili vya Dunia ulipigwa tena pigo (maumivu) kali sana, wao walikuwa na baruti na pia bomu ya atomiki. Hawezi kustahimili maumivu mengine ya kuzaa. Tukiwa na haya makombora na mengineyo siku hizi, vita moja zaidi itaivurumisha angani, kwa kuwa sasa utakombolewa. Na kutakuwa na dunia mpya. Biblia ilisema kutakuwako.

Chini ya Ujumbe wa kila nabii Israeli ilipata utungu, kwa kuwa hawa manabii wangetokea baada ya wanatheologia na wahubiri kuliweka kanisa lote katika hali ya dhehebu. Na nabii huyo atokeapo akiwa na "BWANA ASEMA HIVI", wao walitikisa makanisa hayo nalo likawa na utungu. Hatimaye, alipata utungu wa kuzaa mpaka akajifungua Mwana wa Injili, ambaye alikuwa Neno Lenyewe lililofanyika mwili.

10 Kwa hiyo kanisa kweli liko katika utungu wa kuzaa usiku huu, tena, kwa ajili ya ukombozi wa Mwana, Mwana wa Mungu kuja tena. Wanatheolojia wetu wote, mifumo yetu yote, madhehebu yetu yote, yameoza moja kwa moja toka chini yetu. Kwa hiyo sisi tuko katika utungu wa kuzaa, na Ujumbe kutoka kwa Mungu kila mara unalitupa kanisa katika maumivu mazito zaidi, lakini baada ya kitambo kidogo litamzaa Bibi-arusi. Hilo litamleta Yesu Kristo kwa Bibi-arusi Wake.

Na, halafu, nikifikiri mtu huyu alikuwa hakubaliani nami sana. Nilipokuwa nikiinuka kuhubiri Ujumbe huu, nilifungua Biblia yangu, kupata ukurasa huo.

Na mke wangu alikuwa ndiyo kwanza anipe Biblia mpya, kwa ajili ya Krismasi. Biblia yangu ya kale ina umri wa miaka kama kumi na mitano, na ilikuwa karibu imeraruka vipande-vipande. Kurasa zile, kila wakati ningeifungua, zingepeperushwa toka humo. Na, lakini nilijua mahali tu pa kupata kila Andiko, kwa hiyo ninachunguza kwa makini katika Biblia hiyo. Nami nilichukua tu ile mpya, kwa sababu hiyo nyingine ilionekana imechakaa sana, kwenda nayo kanisani.

11 Na wakati nilipoanza kufungua katika Yohana Mtakatifu, ambapo Maandiko yalipatikana, nilianza kusoma sura ya 16, na aya niliyokuwa nikitafuta haikuwapo. Kwa hiyo nikawaza, "Ajabu!" Nikarudia tena kufungua; bado haikuwepo.

Na Ndugu Jack Moore, kutoka Shreveport, Louisiana, rafiki yangu msiri, alikuwa ameketi pale. Nikasema, "Ndugu Jack, hilo halipatikani katika Mtakatifu Yohana 16?"

Akasema, "Naam."

Na huyu kasisi wa Katoliki aliinuka toka kwa kiti chake, toka kwa kundi la karibu wahubiri wapatao mia moja walioketi jukwaani, akaondoka akaja karibu nami, akiwa amevalia joho lake rasmi na mavazi na misalaba na vinginevyo, na akaja karibu nami. Naye akasema, "Mwanangu, uwe imara. Mungu yu karibu kutenda kazi."

Nikawaza, "Askofu Mkatoliki akiniambia jambo hilo?"

Akasema, "Soma kutoka kwenye Kitabu changu."

Nami nilisoma Maandiko kutoka katika Kitabu chake, na kuchukua somo langu na kuendelea, nikahubiri somo langu.

Baadaye, nilipomaliza, yeye alisimama baada ya mimi kuondoka, na kusema, "Kuna jambo moja linalopaswa kutukia. Baada ya hayo, kanisa halina budi kutoka katika machafuko lililo ndani yake, la sivyo itatubidi kutoka kwenye machafuko ya kanisa." Kwa hiyo, moja ama lingine.

12 Nami nilikuwa nikienda zangu nyumbani, nikarudi Tucson, jioni hiyo. Watoto walikuwa wakililia sandwichi, nami nikasimama kupata sandwichi kwenye stendi ndogo. Ndipo mke wangu akasema, "Bill, sijawahi kuwa na wasiwasi sana maishani mwangu mwote, kukuona umesimama pale ukipapasa —papasa katika Biblia hiyo." Kasema, "Je! Haikukufanya uwe na wasiwasi?"

Nikasema, "La." Nikasema, "Nilijua ilikuwa mle mahali fulani. Hawakuwa na ukurasa huo. Ni kosa la uchapishaji."

Naye alisema, "Kudhani kuwa nilikupa Biblia hiyo. Ilionekana kana kwamba kila jicho mle ndani lilikuwa moja kwa moja juu yangu."

Nami nikasema, "Vema, usingeweza kuzuia hilo. Hilo lilikuwa kosa la uchapishaji wa Biblia." Nilisema, "wao hawakuweka ukurasa huo humo."

Vema, nikashuka na kuliangalia tena, kikamilifu kabisa ilivyoweza kuwa; lakini sura ya 16 inaishia, sehemu, sehemu yake yapata inchi tatu kutoka chini, kwenye mlango wa 17 upande wa pili, inafanya jambo lile lile. Na, kwa kuwa ni Biblia mpya, kurasa hizo mbili zilikuwa zimeshikamana kikamilifu, nami nilikuwa nikisoma kutoka mlango wa 17 badala ya wa 16. "Vema," nikasema, "hiyo ni sawa. Lina kusudi fulani."

13 Na kwa uwazi tu kama ungeweza kusikia sauti yoyote, Sauti ilinijia, na kusema, "Aliingia Nazareti, mahali alipolelewa; kisha akaingia katika sinagogi, kama ilivyokuwa desturi Yake. Ndipo kuhani akampa Maandiko asome, Naye akasoma Isaya 61. Naye alipokisoma kile Chuo, akaketi chini, na kumrudishia kuhani Biblia, kile Chuo, na akaketi chini. Na macho yote ya kusanyiko yalikuwa juu Yake. Na Maneno ya thamani yakatoka kinywani Mwake.

Naye akasema, 'Leo Maandiko haya yametimia.'" "Leo Maandiko haya yametimia."

Namna Maandiko yalivyo sahihi! Ikiwa utachunguza hili katika Isaya 61:1-2 ndipo ambapo Bwana wetu alikuwa akisoma kutoka—Isaya 61:1-2. Lakini katikati ya kifungu cha 2 cha Isaya 61, Yeye alikoma. Ambapo ilisema, "Roho ya Bwana i juu yangu kutangaza mwaka uliokubaliwa." Ndipo Yeye alikoma. Kwa nini? Sehemu ile nyingine, kuleta hukumu, haikuhusika na kuja Kwake mara ya kwanza, bali Kuja Kwake mara ya pili. Mnaona, haikuhusika pale. Jinsi ambavyo Maandiko hayakosei kamwe! Wao daima ni wakamilifu. Yesu alikomea tu ambapo Maandiko yalikomea, kwa kuwa hayo ndiyo hasa yale yalihitajika kuthibitishwa katika siku Zake, sasa, katika kule kuja kwa kwanza. Kuja kwa pili Yeye ataleta hukumu juu ya nchi; lakini si wakati huo. Alipaswa "kuhubiri mwaka unaokubalika."

14 Angalia Masihi akisimama jukwaani, kujitambulisha Mwenyewe na Neno la ahadi kwa wakati huo. Ni ajabu jinsi gani, Masihi akisimama mbele ya kanisa! Na tazama Maneno haya ya thamani, wakati anaposema hapa, "Kuhubiri mwaka unaokubalika."

"Mwaka unaokubalika," kama sisi sote tunavyojua, kama wasomaji wa Biblia, ulikuwa ni "mwaka wa yubile." Kwamba, wakati watumwa wote na wafungwa, kama walivyokuwa, wamechukuliwa mateka, gerezani; na iliwapasa kutoa mwana, kulipa deni; ama binti, kulipa deni, [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] nao walikuwa utumwani. Haidhuru walikuwa wamefungwa utumwani kwa muda gani, ama walipaswa kukaa mle kwa muda gani; mwaka ulipowadia, wa yubile, wakati baragumu ilipolia, kila mtu angeweza kuwa huru kama alitaka kuwa huru. [Sehemu tupu kwenye kanda.] Uko huru. Hukuwa mtumwa tena.

Lakini kama ulitamani kubakia mtumwa, basi ilikubidi upelekwe hekaluni, usisimame karibu na kizingiti cha hekalu, nao walichukua msharasi na kutoboa shimo sikioni mwako, na ndipo ilikupasa kumtumikia huyo mwenye watumwa siku zako zote.

15 Ni mfano mkamilifu ulioje wa Injili ya Yesu Kristo! Unapohubiriwa, ule wakati uliokubalika na wakati wa Sikukuu, mtu ye yote, haijalishi u nani, u wa rangi gani, u wa dhehebu gani, umejizamisha kilindi gani dhambini, au shida yako ni nini, waweza kuwa huru usikiapo ile—ile baragumu ya Injili ya Mungu ikilia! Uko huru!

Bali kama ukiupa Ujumbe kisogo na kukataa kuusikia, tazama, ulitobolewa sikioni, kwa msharasi. Hiyo inamaanisha, kusema, ya kwamba umevuka mpaka kati ya neema na hukumu, na hutasikia Injili tena. Kamwe hutaenda mbali zaidi. Lazima uwe mtumwa kwa dhehebu uliLomo maishani mwako mwote, ukikataa kusikia ule mwaka uliokubaliwa.

Sasa, ile sehemu nyingine yake, kama nilivyosema, haikuhitajika ijibiwe, kwa kuwa Masihi huyu ajaye, wakati wa sasa ni wakati ambapo Yeye ataleta hukumu.

16 Sasa, watu hao wangewezaje kushindwa kuona kwamba Yeye alikuwa ni Nani? Walikosaje jambo hilo? Ingewezekanaje, wakati ilifanywa dhahiri sana na kuonyeshwa? Wangewezaje kamwe kukosa kuona? Wakati Yeye …

Ni Neno iliyoje! Wazia jambo hilo, "Leo Maandiko haya yametimizwa mbele ya macho yenu." Ni nani aliyesema jambo hilo? Mungu Mwenyewe, Ambaye ni mfasiri wa Neno Lake Mwenyewe. "Leo hii Maandiko haya yametimizwa." Masihi, Mwenyewe, akisimama mbele ya kusanyiko na kusoma Neno kutoka katika Biblia, linalohusu Yeye Mwenyewe, kisha akisema, "Leo Maandiko haya yametimia," nao wangali walishindwa kuliona.

Ingekuwa msiba ulioje, lakini imetendeka. Limetukia mara nyingi. Ingewezekanaje? Hakika, kama ilivyofanyika nyakati zingine, kwa kuamini tafsiri ya watu Neno. Hilo ndilo lililosababisha jambo hilo. Hao waaminio katika siku hizo, wanaojiita waamini, walikuwa wakichukua tafsiri ya yale kuhani aliyokuwa amesema juu ya Maandiko. Kwa hivyo Yesu akiwa hana cheo cho chote au kuwa katika vyama vyao, Yeye alifukuzwa toka kwa kundi lao.

Na kwa hivyo, wao hawangejitambulisha naye, kwa kuwa Yeye alikuwa tofauti nao. Utu wa Yesu Kristo ulikuwa wa kipekee sana hivi kwamba hakuna mtu aliyepaswa kukosa kuona kwamba huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu, kwa sababu Yeye alikuwa ni utambulisho mkamilifu wa Maandiko yaliyoandikwa juu Yake.

Hivyo ndivyo Mkristo yeyote anavyojulikana, wakati maisha yake yanapotambulisha mambo hasa ambayo Mkristo anapaswa kufanya.

17 Jinsi ambavyo angeweza kusimama pale na kusema, "Leo Maandiko haya yametimizwa mbele ya macho yenu!" Ni bora iliyoje, ni dhahiri iliyoje, na hata hivyo watu hao walielewa vibaya. Kwa nini? Ni kwa sababu walichukua tafsiri ya utaratibu fulani wa makuhani waliokuwa wakiusikiliza.

Na historia daima inajirudia. Maandiko huwa na maana zaidi ya moja na ufunuo zaidi ya mmoja.

Kwa mfano, kama inavyosema katika Biblia, ya kwamba, "Kutoka Misri nimemwita mwanangu," ikimaanisha Yesu. Tazama kandoni mwa karatasi kuhusu hilo na utatambua kuwa pia linamtaja Yakobo—Andiko lile lile. Yesu alikuwa Mwana Wake mkuu sana. Yakobo alikuwa ni mwanawe ambaye alimwita kutoka Misri, ambaye marejeo ya Scofield na marejeo mengine yote yanaelezea jambo hilo, kwa sababu hayo ni Maandiko yaliyokuwa yakirejelea. Kwa hiyo ilikuwa na—na jibu maradufu; ilikuwa na jibu kwa Yakobo aliyeitwa, na kwa Yesu aliyeitwa.

Na ndivyo ilivyo leo! Ni kwa sababu sisi tuko katika machafuko kama tulivyo, na watu wanashindwa kuona Ukweli wa Mungu, ni kwa sababu kuna tafsiri nyingi sana za mwanadamu za Neno la Mungu. Mungu hahitaji mtu ye yote kufasiri Neno Lake. Yeye ni mfasiri Wake Mwenyewe.

18 Mungu alisema, hapo mwanzo, "Iwe nuru," na ikawa nuru. Hilo halihitaji tafsiri.

Yeye alisema, "Bikira atachukua mimba," naye akachukua mimba. Hilo halihitaji tafsiri yo yote.

Wakati … Fasiri ya Mungu ya Neno Lake ni wakati anapothibitisha na kuhakikisha kwamba ni kweli. Hiyo ndiyo tafsiri Yake, kwa kuifanya itimie. Hapo ndipo fasiri ya Mungu ilipo, ni wakati anapolifanya Neno Lake kutimia. Yeye anakufasiria jambo Hilo.

Kama kwamba kamwe hakujakuwako na nuru, Naye akasema, "Iwe nuru," na ikawa, hiyo haihitaji mtu ye yote kufasiri.

Bali tunachanganya mifumo ya kujitengenezea ndani Yake, na, unapofanya hivyo, u—unaliondoa kwenye mstari. Daima imekuwa hivyo.

19 Lakini bado ninawazia lilikuwa la kushangaza iliyoje. Wazia jambo hilo, Yule Masihi! Kwa nini walishindwa kumwona? Kwa sababu, viongozi wao hasa ambao walipaswa kumjua Yeye, ambao walipaswa kujua Maandiko, waliopaswa kuwa na ufahamu wa Maandiko, walimdharau Mtu huyu na kusema, "Yeye ni mtoto haramu, kwa—kwanza Tusingeamini jambo Hilo."

Miaka kadhaa baadaye, hatuamini jambo hilo. Tungekufa kwa kusudi la kusema ya kwamba Yeye alikuwa Mwana aliyezaliwa na bikira.

Na siku moja itakuwa kwamba mambo yale tuonayo Yehova akifanya leo, wanadamu kwa nyakati zijazo, kama zitakuwapo, watakufa kwa ajili ya jambo hili tunaloongea leo. Itakubidi kufanya hivyo wakati ile alama ya mnyama itakapokuja, wala huruhusiwi kuihubiri Injili hivi. Wakati muungano mkuu wa makanisa utakapoungana, ambao uko sawa sasa hivi kwa ajili ya kanisa la ulimwengu, itakubidi kutia muhuri ushuhuda wako kwa maisha yako mwenyewe, kwa Hili.

20 Huna budi kuliamini sasa. Ikiwa makuhani wale waliomhukumu Yeye wangefufuka, hawangemhukumu. "Lakini," unasema, "kama ningalikuwa kule, ningalifanya hivi na vile." Vema, huo haukuwa ni wakati wako. Lakini, huu ni wakati wako, huu ndio wakati.

Unasema, "Vema, kama Yeye alikuwa hapa!"

Biblia ilisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele," yeye yule, kwa hiyo Yeye yuko hapa. Lakini, Yeye yupo hapa. Kwa kuwa ulimwengu umestaarabika, umekuwa mkuu zaidi, na umeelimika zaidi; Yeye yuko hapa katika umbo la Roho, ambayo hawawezi kuiua wala kuiweka mautini. Alikufa mara moja; Hawezi kufa tena. Ilimbidi afanyike mwili kusudi Mungu auawe katika mwili, kwa ajili ya dhambi. Lakini wakati huu asingeweza kamwe kufa; Ni Roho Mtakatifu.

21 Sasa, namna ya kuwaza kuwa wao walikuwa na mambo hayo dhidi Yake. Jambo lingine, ya kwamba Yeye hangejiunga na vyeo vyo vyote vya vyeo vyao. Halafu, mnaona, hilo bado lilimfanya mtu mbaya. Yeye asingejiunga na—na madhehebu yao, asingejiunga na ukuhani wao, wala asingekuwa na uhusiano wowote nayo. Halafu basi, mbali na hayo yote, Yeye alijaribu kubomoa kile walichokuwa wamejenga.

Aliingia hekaluni. Tunamwita Mtu mpole; Yeye alikuwa hivyo, lakini mara nyingi tunaelewa vibaya upole.

Yeye alikuwa ni Mtu mwenye huruma, lakini hata hivyo tunashindwa wakati mwingine kuelewa huruma ni nini. Si huruma ya kibinadamu, si huruma. Lakini, *huruma* ni "kufanya mapenzi ya Mungu."

Yeye alipitia karibu na birika ya—ya Bethzatha, lile lango. Pale walilala watu, umati wa watu. Umati wa watu si idadi fulani. Lakini kulikuwako wingi wa watu; viwete, vipofu, vilema, waliopooza. Naye aliwahurumia watu, daima. Naye akaenda kwa mtu mmoja ambaye hakuwa kiwete, kipofu, kilema, wala

aliyepooza; labda alikuwa na ugonjwa wa tezidume, labda alikuwa na udhaifu mdogo ambao ulikuwa sugu. Alikuwa nao miaka thelathini na minane. Haungemsumbua, haungemwua. Yeye alikuwa amelala kwenye machela. Naye alisema, "Wataka kuwa mzima?"

Na mtu yule akasema, "Sina ye yote wa kunitia majini, lakini wakati ninapokuja mimi, naam, mtu mwingine hushuka mbele yangu." Mnaona, hangeweza kutembea, hangeweza kuona, hangeweza kuzunguka, bali alikuwa mnyonge tu.

Naye Yesu akamwambia, "Simama. Chukua kitanda chako uende nyumbani kwako. Naye Yesu aliulizwa juu ya jambo hilo, kwa kuwa mnakumbuka Maandiko yalisema hivi.

22 Si ajabu! Kama angekuja Jeffersonville usiku wa leo na kufanya tendo kama hilo, bado wangezungumza habari Zake.

Lakini, kumbukeni, Yeye alikuja kufanya jambo moja, lilikuwa ni mapenzi ya Mungu. Sasa, hilo linapatikana katika Yohana Mtakatifu 5:19, utapata jibu. Yeye alisema, "Amini, Amin nawaambieni, Mwana hawezi kufanya lo lote Mwenyewe ila lile Yeye aonalo Baba akitenda, hilo Mwana analitenda."

Sasa, walipaswa kujua ya kwamba hilo lilikuwa ni thibitisho lenyewe la unabii wa Musa, "Kwa kuwa Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama mimi."

Je! Uliona, wakati alipomwona mtu huyo, Yeye alisema … Yesu alijua ya kwamba alikuwa katika hali hii kwa miaka mingi. Mnaona, Yeye akiwa Nabii, alimwona mtu yule kwa hali hiyo na akaenda chini pale na kuyumba—kuyumba kati ya watu hao, akipenyeza kati ya kundi, hadi Yeye akampata mtu fulani.

Alipita viwete, vilema, vipofu, na waliopooza, hata hivyo ni Mtu aliyejaa huruma. Lakini, *huruma* ni "kufanya mapenzi ya Mungu."

23 Sasa, tunamwona, kwa kuwa hangeungana nao, asingekuwa na cho chote cha kufanya katika vyeo vyao, basi Yeye alikuwa ametengwa. Asingekuwa na cho chote…

Mbali na hayo, Yeye aliingia hekaluni siku moja. Mtu yule aliingia humo na kuona nyumba ya Mungu imeoza tu kama ilivyo siku hizi. Walikuwa wakinunua, wakiuza, wakibadilisha fedha. Naye akageuza meza zao za pesa, akachukua kamba na kuzisokota na kuwachapa wale wabadili fedha toka mle hekaluni Ndipo akawaangalia kwa hasira, na kusema, "Imeandikwa," haleluya, "Nyumba ya Baba Yangu ni nyumba ya maombi; nanyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi. Nanyi, kwa mapokeo yenu, mmetangua amri za Mungu."

Loo, kundi kama hilo lingeweza kamwe kumwamini? La, bwana. Walikuwa wamepakwa matope ya nguruwe katika uchafu wa jamii na uchafu wa siku hizo, hata walikuwa wamegandamizwa sana kidini hata wasingeweza kusikia mitetemeko ya Nguvu za Mwenyezi Mungu. Si ajabu maskini mwanamke huyo angeweza kugusa vazi Lake na kuponywa nalo; na askari mlevi angeweza kumtemea mate usoni Mwake na asione nguvu yo yote! Inategemea jinsi unavyoliendea. Inategemea unatafuta nini. Unapoenda kanisani, inategemea unatafuta nini.

24 Sasa tunamwona amesimama pale. Bila shaka watu walikuwa wamemwonya, walimwonya—makuhani walikuwa wamewaonya watu, "Sasa yeye yuaja hapa Sabato ijayo, na akija msimsikize. Sasa, huenda ukaenda na ukaketi hapa, lakini usijali yale anayosema, kwa sababu Yeye si wa kundi letu. Yeye ni aliyetengwa. Hana kadi ya ushirika. Yeye hata hana kijikaratasi cha dhe—dhehebu. Yeye hana kitu kama hicho."

"Yeye ni nani?"

"Kijana fulani mkorofi aliyezaliwa chini pale mwana haramu, nyumbani mwa seremala, ambaye mama yake alipata mimba kabla hawajaoana, nao wanajaribu kuficha hilo kwa kutumia jambo la kimbinguni.

"Tunajua ya kwamba, wakati Masihi atakapokuja, Yeye atashuka kwenye njia za Mbinguni na kumwendea kuhani wetu mkuu na kusema, 'Mimi hapa, Kayafa.'" Lakini tunaona ya kwamba Yeye hakufanya hivyo, kwa sababu haikuandikwa katika Neno namna hiyo. Zilikuwa ni desturi za wanadamu zilizowafanya waamini hivyo.

Neno lilikuwa limesema ya kwamba Yeye angekuja jinsi tu Yeye alivyokuja. Naye hapo amesimama, akilisoma Neno, na kuwaambia, "Leo Maandiko haya yametimia machoni mwenu." Na bado wanashindwa kumwona ama kumtambua, kama walivyofanya katika nyakati zingine zote.

25 Nuhu angeweza kusema jambo lile lile, siku ambayo aliingia katika safina na mlango ukafungwa. Musa angeweza kuinua dirisha hilo juu ya safina, akatazama kusanyiko … Kumbuka, Mungu alifunga mlango. Naye angaliweza kusema, "Leo Maandiko haya yametimia machoni mwenu," lakini walikuwa wamechelewa sana wakati huo. Alikuwa amehubiri miaka mia moja na ishirini, kujaribu kuwaingiza kwenye mtumbwi aliokuwa amejenga, akiwaambia ya kwamba Maandiko yalisema, "BWANA ASEMA HIVI, itanyesha," bali

walingojea muda mrefu sana. Lakini Nuhu angeweza kusema kwa urahisi kwamba, "Leo, siku hii, Maandiko yametimia."

Musa, ile ile siku ile Nguzo ya Moto iliposhuka juu ya Mlima Sinai na kutoa ushuhuda wake, Musa angalisema, "Leo Maandiko haya yametimia."

Musa, mwajua, alikuwa mtu aliyeitwa na Mungu, nabii. Na wakati alipokuwa anaitwa, akiwa ni nabii, ilimbidi apate tukio la kimbinguni. Ili awe nabii, ilimbidi kukutana na Mungu uso kwa uso na kuzungumza Naye. Na jambo lingine, yale aliyosema ilibidi yatimie, la sivyo hakuna mtu angalimwamini.

Kwa hivyo, hakuna mtu aliye na haki ya kujiita hivyo, hadi ameongea uso kwa uso na Mungu nyuma ya jangwa mahali fulani, ambapo yeye alikutana na Mungu Mwenyewe! Na makafiri wote ulimwenguni hawangemshawishi alitupilie mbali; yeye alikuwa pale, naye alijua ilitendeka. Kila Mkristo anapaswa kuwa na tukio hilo kabla hawajasema lolote kuhusu kuwa Mkristo. Uzoefu wako mwenyewe!

26 Nilizungumza na mpwa wangu, muda mfupi uliopita, mvulana mdogo Mkatoliki, aliyesema, "Mjomba Bill, nimekimbia kutoka kwenye nguzo hadi nyingine, nikienda kila mahali, nikijaribu kupata kitu fulani." Usiku baada ya usiku, kabla mkutano huu haujaanza, amekuwa akilia. Na wakati wa usiku, yeye amekuwa akiota ndoto ya kuingia, akikimbia madhabahuni, panapohubiriwa, na kufanya maungamo kuwa amekosa.

Nikasema, "Melvin, haidhuru unajaribu kwenda wapi, unajiunga na makanisa mangapi, unasema ni 'Salamu ya Maria,' ama unapata baraka ngapi kutoka kwa mwanadamu, huna budi kuzaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu. Ndicho kitu pekee kitakachoridhisha moyo wa mwanadamu."

Hiyo ni, ninajua wana kibadala, leo, cha kuzaliwa mara ya pili, peana tu mikono na mhubiri na uandike jina lako kwenye kitabu. Lakini, enyi marafiki, hilo ni fundisho la sharti. Si Ukweli wa Biblia. Kama ingekuwa hivyo, Matendo ya Mitume, katika mlango wa 2, italazimika kusoma hivi, "Siku ya Pentekoste ilipotimia kikamilifu, mchungaji alitoka akaenda na kupeana mikono na watu."

Lakini ilisema, "Hata ilipotimia Siku ya Pentekoste," wakati wa kuanzishwa kwa kanisa, "kukaja uvumi toka Mbinguni kama uvumi wa upepo ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi!" Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyokuja mara ya kwanza. Hivyo ndivyo alivyokuja kila wakati tangu wakati huo. Yeye ni Mungu, wala habadiliki. Sasa, huwakwaza watu.

Wanasema, "Hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya siku nyingine."

27 Vema, ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kila wakati Kanisa lilipompokea Roho Mtakatifu, daima amekuja kama alivyofanya mara ya kwanza, chini ya maagizo yale yale, Matendo 2:38; kamwe haijabadilika, kamwe haitabadilika.

Kama vile maagizo ya daktari ya ugonjwa. Yeye ataandika maagizo ya ugonjwa, daktari anaandika. Ka kuwapelekea wengine wasiofuzu, watoe dawa, anaweka nyingi ya dawa inayoharibu sumu, itakuwa dhaifu sana na haitakufaidi cho chote. Akiweka sumu nyingi sana ndani yake, itakuuwa. Haina budi kuandikwa tu kulingana na daktari.

Na maagizo ya daktari namna ya kumpokea Roho Mtakatifu tumepewa na Daktari Simon Petro, kwenye Siku ya Pentekoste. "Nitakupa maagizo. Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa maagizo haya ni kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu." Maagizo ya Milele!

28 Musa alikuwa amepata tukio hili. Alishuka akaenda nchini na akaanza kuwaambia watu, "Nilikutana na Nguzo ya Moto. Ilikuwa katika kijiti kilichowaka moto. Naye akaniambia niwaambie, 'MIMI NIKO AMBAYE NIKO. Shuka uende; Nitakuwa pamoja nawe. Chukua ile fimbo mkononi mwako na uinyoshe juu ya Misri; lo lote utakaloomba, litafanyika.'"

Vema, labda kasisi fulani alisema, "Upuuzi!"

Lakini walipoona jambo halisi la hili, likitimia, hawangejizuia tena. Walijua alitumwa na Mungu.

Basi ikiwa Musa alisema yeye aliona hilo na kulishuhudia kuwa Kweli, basi Mungu apaswa, kama hiyo ni Kweli, kutambulisha na kuthibitisha neno la mtu huyo, Kweli! Hiyo ni kweli.

Kama Yesu Kristo alisimama pale na kusoma, siku hiyo, "Leo Neno hili limetimia mbele zenu," Mungu anawajibika kulifanya Neno hilo litimie.

Tunasimama hapa usiku wa leo na kusema, ya kwamba, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Mungu anawajibika kuthibitisha hilo kuwa kweli, kwa sababu ni Neno Lake. Sasa, linafanya nini? Inahitaji imani, katika kuliamini. Inahitaji imani, katika kuliamini Neno Lake, ya kwamba ni Kweli.

29 Angalia kilichotukia wakati Musa alipowatoa hao watoto, na wale wote waliomfuata. Wale ambao

hawakumfuata walikaa Misri. Lakini wale waliomfuata Musa, walipotoka kwenye Bahari ya Shamu na kuingia nyikani, Mungu alishuka juu ya Mlima Sinai. Ile Nguzo ya Moto iliuwasha moto mlima wote, na Sauti ikanena kutoka pale, na Mungu akatoa zile amri kumi.

Musa angaliweza kwenda pale mbele za watu, na kusema, "Leo Maandiko ambayo nimewaambia, kama nabii Wake, yametimia siku hii. Nimewaambia ya kwamba Mungu alikutana nami, na kule juu kwenye kijiti kilichowaka moto, katika Nguzo ya Moto, Naye akasema hivi, 'Nita- … Hii itakuwa ni ishara. Utawaleta watu wale hadi papa hapa mahali hapa tena!' Na pale kuna Mungu katika Nguzo ile ile ya Moto niliyowaambia alikuwamo, ikining'inia pale mlimani. Leo hii unabii huu umetimizwa. Hapa Yeye anathibitisha kuwa mambo yale niliyoyasema ni Kweli."

Mungu na atupe watu wengi zaidi kama hao, walio waaminifu na wanyofu, na waseme Kweli, ili Mungu Mwenyezi angeweza kuthibitisha ya kwamba Neno Lake lingali ni Kweli! Yeye anabaki yeye yule jana, na hata milele. Kwa nini asingefanye hivyo? Yeye aliahidi kufanya hivyo.

30 Huenda Yoshua alisema vile vile, siku aliyorudi Kadeshi-barnea, ambako walikuwa wamesafiri mbali sana jangwani. Walikuwa wakiitilia shaka nchi hiyo kwamba ni nchi ambayo Mungu alisema ingekuwa. Lakini Mungu aliwaambia ilikuwa ni nchi nzuri, ilikuwa ikitiririka maziwa na asali. Na Yoshua na Kalebu ndio wawili tu ambao wangeamini jambo hilo, kati ya hao wengine kumi walioondoka. Waliporudi walikuwa na ushahidi; wao walikuwa na kichala cha zabibu ambazo zingebebwa tu na watu wawili wenye nguvu.

Yoshua na Kalebu wangeweza kusimama papo hapo na kusema, "Leo Maandiko haya yametimia. Huu hapa ushahidi kwamba ni nchi nzuri." Hakika. Kwa nini? "Kuna ushahidi kwamba ni nchi nzuri. Ungepata wapi vitu kama vile, huko Misri? Hakukuwako na mahali kama hapo. Lakini leo hii Maandiko haya yametimia."

Yeye angesema jambo lile, lile lile, wakati alipofanya unabii na kusema kuta za Yeriko zingeanguka baada ya wao kuzizunguka mara saba, siku saba, mara saba kwa siku. Na wakati walipozizunguka zile mara ya mwisho, kuta zikaanguka. Yoshua angaliweza kusimama na kusema, "Siku hii, Amiri Jeshi Mkuu wa jeshi la Bwana aliyeniambia majuma kadhaa yaliyopita ya kwamba lingetukia namna hii, leo Maandiko haya yametimia." Hapo palikuwa na kuta, zimelala ardhini. "Njoni, twendeni tukautwae. Ni mali yetu. Leo Maandiko haya yametimia."

Ni ajabu iliyoje, watu wa Mungu wametetea mambo yaliyo kweli!

31 Israeli, kule mtoni, wakati walipomiliki ile nchi, walivuka. Watafanyaje jambo hilo? Ni mwezi wa Aprili. Mafuriko yanashuka kwa sababu theluji inayeyuka, huko juu katika Uyahudi. Loo, namna ilivyoonekana kana kwamba Mungu alikuwa jemadari ovyo kuwaleta watu Wake chini pale katika mwezi wa Aprili, wakati Yordani ilikuwa imefurika sana kuliko ilivyowahi kuwa. Wakati mwingine …

Huenda ningepaswa kukomea hapa, kama ningekuwa na wakati, kuwatolea tu kidokezo kidogo. Wakati mwingine huenda ungeketi nje pale ukiwa na kansa au huenda umeketi pale ukiwa na ugonjwa, ukiwaza, "Mbona, mimi nikiwa Mkristo, ningekuwa hivi? Kwa nini ningeketi hivi, kama mimi ni Mkristo?" Wakati mwingine Mungu huacha mambo yawe giza sana hata huwezi kuona juu, karibu, au mahali pengine popote, halafu Yeye anakuja na kufanya njia kupitia kwayo, upate kusema, "Leo Maandiko haya yanatimia, kwamba Yeye aliahidi kufanya hivyo."

32 Aliwaacha wana wa Kiebrania waingie moja kwa moja kwenye tanuru ya moto. Walisema, "Mungu wetu anaweza kutuokoa na moto huu katika tanuru. Lakini, hata hivyo, hatutaisujudia sanamu yako." Walipotoka kule, harufu ya tanuru ilikuwa juu yao … hakuna harufu ya tanuru, hasa, juu yao; wangaliweza kusema, "Leo Maandiko haya yametimia."

Wakati Danieli alipotoka kwenye tundu la simba, angaliweza kusema jambo lile lile.

Yohana Mbatizaji. Baada ya miaka mia nne ya mafundisho ya kidini, si ajabu kwamba kanisa lilikuwa limechanganyikiwa wakati huo! Wakati alipotokea nyikani, Yordani, angaliweza kusimama papo hapo ukingoni, kama alivyofanya, na kusema, "Leo Maandiko haya, Isaya 40, yametimia."

33 Jinsi ambavyo ningeweza kusimama hapa na kuwaambia yale kasisi huyo mzee aliniambia! Kasema, "Mwanangu, hukumaliza Ujumbe huo kamwe."

Nikasema, "Tulieni."

Akasema, "Unamaanisha hao Wapentekoste hawaoni jambo hilo?"

Nikasema, "La."

Yeye akasema, "Nayafahamu." Na kuhani Mkatoliki, pia! A-ha. Akasema, "Kwa nini hukuendelea?"

Nikasema, "Tulieni."

Yeye alisema, "Utukufu kwa Mungu! Nayafahamu."

Na yapata wakati huo Roho Mtakatifu alimshukia dada yake, ameketi pale mkutanoni. Naye akainuka, akinena katika lugha zisizojulikana, na kutoa tafsiri ya jambo lile lile kasisi yule nami tulikuwa tukinena, jukwaani! Kanisa lote, mahali pote, likaingia katika kishindo. Na habari zake zikaendelea katika mkutano wa Oral Robert juma lililopita, au majuma mawili yaliyopita, na zikawa ndizo mazungumzo katika mkutano huo. Namna ambavyo kuhani huyo … Akiwa ameketi chini ya Roho Mtakatifu, aliyefunuliwa huko nje kupitia kwa mwanamke, dada yake naamini alikuwa, juu ya yale yaliyokuwa yakitendeka kule jukwaani, na akafunua kitu hicho tulichokuwa tukificha.

Saa ile tunayoishi, leo Maandiko haya yametimia. Leo hii Nuru za jioni zimekuja, nasi tunashindwa kuiona. Angalia.

34 Yohana alisema, "Leo mimi ni 'sauti ya mtu aliaye nyikani,' kama nabii Isaya alivyosema. Itengenezeni njia ya Bwana!"

Hawakumwelewa. Sema, "Loo, wewe ni Yesu … wewe—wewe ni Kristo," hasa.

Yeye alisema, "Mimi siye Kristo." Yeye alisema, "Mimi sistahili kufungua viatu Vyake. Lakini," akasema,"Yeye amesimama miongoni mwenu, mahali fulani," kwa kuwa alikuwa na hakika ya kwamba angekuwako. Angekuwa katika siku yake, maana Mungu alimwambia angemtambulisha Masihi.

Siku moja kijana mwanamume alikuja akitembea kupitia pale, naye akaona kama Nuru juu Yake, ishara. Naye akapaza sauti, "Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu! Leo hii Maandiko haya yametimia mbele yenu." Hakika.

35 Kwenye Siku ya Pentekoste, namna Petro alivyosimama na kunukuu Maandiko yao, ya Yoeli 2:38. Wakati, wao wote walikuwa wakicheka, hao watu. Wasingeweza kuzungumza katika lugha yao wenyewe. Walikuwa wakigugumiza kitu kingine. Biblia ilisema "Ndimi zilizogawanyikana." Kugawanyika ni ndimi zilizotawanyika, si kusema lo lote, kugugumiza tu, Wakikimbia huku na huko kama kundi la walevi!

Wote walisema, "Vema, watu hawa wamelewa. Waangalie, angalia namna wanavyotenda, namna hao wanawake na wanaume. Wao ni wavivu," kasema kundi hilo la kidini la siku hizo.

Petro akasimama katikati yao, akasema, "Waume na ndugu zangu, ninyi mkaao Yerusalemu, nanyi mkaao katika Uyahudi, na ijulikane kwenu ya kwamba hawa hawakulewa, kama mnavyodhania, kwa kuwa ni saa tatu ya mchana. Lakini hili ndilo lile lililonenwa na nabii Yoeli, 'Itakuwa katika siku za mwisho, nitamwagia watu wote Roho Yangu.' Leo hii Maandiko haya yametimia." Hakika.

36 Luther alikuja kwa wakati unaofaa. Wesley alikuja kwa wakati unaofaa. Pentekoste ilikuja kwa wakati unaofaa. Hakuna kitu kilicho nje ya utaratibu.

Sasa ninawaomba mtafakari wakati na saa tunayoishi sasa, pamoja na Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hizi. Kama huko nyuma katika nyakati zingine, watu wangeweza kusema, "leo Maandiko haya," "leo Maandiko haya," basi vipi kuhusu Maandiko ya siku hii? Ni kitu gani kilichoahidiwa kwa ajili ya siku hii? Tunasimama wapi? Tunaishi katika wakati upi, saa inapogonga, ile saa ya kisayansi, usiku wa manane kasoro dakika tatu? Ulimwengu una mizaha. Kanisa liko katika kitanda cha uharibifu. Hakuna mtu anayejua mahali wanaposimama. Ni saa ngapi za mchana? Vipi kuhusu Maandiko ya siku hii? Hali za kanisa, ama, hali za kanisa leo!

37 Ulimwenguni, siasa, mfumo wetu wa ulimwengu, umeoza uwezavyo. Mimi si mwanasiasa. Mimi ni Mkristo. Lakini, sina shughuli ya kuzungumza juu ya siasa, bali nataka tu kusema zimeoza pande zote mbili.

Nilipiga kura mara moja, hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya Kristo; Sina budi kushinda. Shetani alipiga kura dhidi yangu, na Kristo alinipigia mimi. Yategemea wapi ninatupa kura yangu. Nafurahi nimemtupia Yeye; acha ulimwengu useme watakalo. Ningali ninaamini ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye atathibitisha jambo hilo. Hakika Yeye atafanya hivyo. Hakika.

Kuongezeka kwa uhalifu, uhalifu wa vijana!

Angalia taifa letu, wakati mmoja ua la dunia. Demokrasia yetu kuu ilianzishwa huko nyuma katika—katika … kwenye azimio la uhuru. Na tangazo la uhuru lilitiwa sahihi, nasi tulikuwa na demokrasia. Na babu zetu wakuu, na mambo waliyofanya; tulikuwa na taifa kuu.

Lakini sasa linaoza, na kuporomoka, na kutetemeka, na kuachilia. Na kujaribu kulipiza watu kodi wapate pesa watume ng'ambo kule kununua urafiki kwa adui; wao wanazitupa nyuma usoni petu. Vita vya kwanza vya dunia, vita vya pili vya dunia, na hali ukiendelea kwa vile vya tatu. Hakika. Siasa zimeoza, zimeharibika, zimeoza mpaka chini. Ni vile hasa Mathayo 24 ilivyosema ingekuwa, "Taifa lingeshindana na taifa, ufalme dhidi ya ufalme." Mambo haya yote yangetukia. Hebu na tuchunguze

jambo hili sasa. Vema.

38 Tazameni lingine: kuongezeka kwa utafiti wa kisayansi. Sasa, wakati mmoja, ninii tu … Babu yangu alienda kumwona bibi yangu, katika gari la ng'ombe. Sasa ni eropleni aina ya jeti, au hata mzunguko angani, hadi anga za juu Sana. Ni kuu … Vipi, ni nani aliyesema jambo hili? Danieli 12:4, ilisema, "Maarifa yataongezeka katika siku za mwisho." Tunaona saa tunayoishi. Angalia sasa vi—hali za ulimwengu, hali ya sayansi.

Na angalia tena, leo, katika mfumo wetu wa elimu. Sasa msijaribu kukana jambo hili. Nina vipande vya magazeti, vikifundisha ngono katika kani … shuleni mwetu, ya wanafunzi wadogo kufanya mapenzi, kuona kama wanaweza kuoana ulimwenguni. Naam, bwana.

Vipi kuhusu ukuhani wetu? Usiku wa leo nimepata kipande kutoka kwenye karatasi. Kule Los Angeles, California, ambako kundi la makasisi, Wabatisti na Wapresbiteri, wahudumu, waliingiza kundi la walawiti na kufanya ulawiti, wakisema wao walikuwa wakijaribu kuwaleta kwa Mungu. Wakati, hiyo ni moja ya laana za wakati huo, Msodoma! Na sheria hata iliwaweka chini ya ulinzi.

39 Sasa tuko wapi? Mfumo wetu wote umeoza kutoka chini yetu. Niliona ongezeko la ulawiti kote Marekani limeongezeka asilimia ishirini ama thelathini zaidi ya mwaka jana. Wazia jambo hilo, mwanaume akiishi na mwanauame, kama tu vile walivyofanya Sodoma.

Kuongezeka kwa uhalifu, uhalifu wa watoto! Tunaishi wakati gani? Leo hii Neno hili la unabii limetimia.

Ulimwengu wa kidini, kanisa lenyewe, kanisa lile, kanisa lile lililoitwa litoke tunaloita kanisa lililoitwa litoke, ule wakati wa kanisa la mwisho, wakati wa kanisa la Kipentekoste, uko wapi? Uko katika Laodikia, kama Maandiko yasemavyo.

Leo hii wameachilia vizuizi. Wanawake wao wamevaa nusu. Watu wao ni … Ni jambo la kutisha sana. Wengine wao walioa mara tatu ama nne, kwenye halmashauri za mashemasi, na kila kitu kingine. Wameachilia, na kuleta uharibifu, kwa sababu wamekaa katika mabaraza na kuchukua mahali pamoja na ulimwengu.

Na, leo, wana majengo bora kuliko waliyowahi kuwa nayo. Mahali fulani, mmoja wao anajenga ukumbi wa dola milioni hamsini, dola milioni hamsini. Wapentekoste! Ilikuwa huko chini pembeni, miaka ishirini na mitano iliyopita, ikipiga tari. Kasema, "Sisi …"

Kwa sababu, Maandiko yalisema, katika Ufunuo 3, ya kwamba wewe ni "'Tajiri,' kasema, 'Mimi ni tajiri. Ninaketi kama malkia. Sina haja ya kitu.' Wala hujui ya kwamba wewe u mnyonge, mwenye mashaka, maskini, uchi, kipofu, wala hujui!"

Leo hii Maandiko haya yametimia machoni mwenu. Amina! Amina maana yake ni "na iwe hivyo." Sijifanyii mwenyewe amina, lakini namaanisha naamini kuwa ni Kweli. Leo hii Maandiko haya yametimia.

40 Kanisa la Kipentekoste liko katika hali ya Laodikia. Loo, wangali wanaruka na kupaza sauti, na kuendelea wakati muziki unapopigwa. Muziki ukomapo kuchezwa, au ule mdundo wa kucheza ngoma wengine wao hucheza na kuuita Ukristo, na huo ukomapo, utukufu wote umekwisha. Naam.

Ikiwa ni kutukuza Mungu halisi, hakuna filimbi za kutosha na nguvu za kutosha ulimwenguni kukukomesha. Wakati kutukuza kwa kweli kuna toka kwa Mungu, hakuhitaji muziki kuchezwa; Kunahitaji Roho wa Mungu kushuka juu yake. Huko ndiko kunakofanya jambo hilo.

Nao walilisahau zamani, kwa kuwa wao waliweka kipimo cha kipawa cha Roho Mtakatifu kuwa, "ishara halisi ni kunena kwa lugha." Nami nilisikia pepo na wachawi wakinena kwa lugha.

Roho Mtakatifu ni Neno la Mungu ndani yako, ambalo hujitambulisha Lenyewe kwa kulikubali Neno hilo. Mbali na hilo, hawezi kuwa Roho Mtakatifu. Ikiwa asema ni Roho Mtakatifu na anakana neno la Biblia hiyo, hawezi kuwa ni Roho Mtakatifu. Huo ndio ushahidi kama unaamini ama huamini.

41 Angalia ishara nyingine kuu. Wayahudi wako katika nchi ya uenyeji wao; taifa lao wenyewe, fedha zao wenyewe, mwanachama wa Umoja wa Mataifa. Wao wana jeshi lao wenyewe. Wana kila kitu. Wako katika nchi ya uenyeji wao; ambapo, Yesu alisema, "Jifunzeni mfano wa mtini." Hao hapo, wamerudi moja kwa moja katika taifa lao. Leo hii Maandiko haya yametimizwa, Wayahudi katika nchi ya uenyeji wao.

Leo hii Maandiko haya yametimia, Wakati wa Kanisa la Laodikia.

Leo hii Maandiko haya, Mathayo 24, yametimia. Ulimwengu uko katika uharibifu, kitu hicho chote; mataifa dhidi ya mataifa, matetemeko ya nchi mahali mbalimbali, tufani kuu zikishuka, zikiyatikisa mataifa, na kadhalika, majanga makubwa kila mahali. Leo hii Maandiko haya yametimia.

42 Sasa tuliona hali ya ulimwengu. Tunaona mahali ambapo kanisa la kawaida, la kawaida … Mashirika, madhehebu, tunaona mahali walipo. Tunaona mahali mataifa yalipo. Nasi tunaona ya kwamba siku hizi

ahadi hizi zimetimia.

Sasa, lakini katika siku hii atakuja Mzao wa Kifalme wa Ibrahimu. Hivyo ndivyo hasa ingekuwa, angekuwa Bibi-arusi wa Kifalme kwa Mwana wa kifalme, aliyeahidiwa. Kama nilivyosema jana usiku, haitakuwa ni mbegu ya kawaida, itakuwa ni Mbegu ya kiroho. Kutakuwako na Bibi-arusi wa kiroho atakayeinuliwa, ambaye atakuwa Mzao wa Kifalme wa Imani ya kifalme ya Mwana wa Kifalme wa Ibrahimu. Yeye atakuja jukwaani katika siku za mwisho, na wakati na mahali ni ahadi aliyopewa.

Kulingana na Malaki 4, Maandiko, kutakuwako na Ujumbe utakaotikisa mioyo ya watu iwaelekee baba zao wa kimitume tena. Kuna mmoja atakayeinuka, katika nguvu za Eliya, atakayeinuka; mtu wa jangwani atakayekuja, na atakuwa na Ujumbe ambao utarudi moja kwa moja kwenye Neno tena. Hiyo ndiyo saa tunayoishi.

43 Halafu, fikiria sasa, nawaulizeni katika saa hii, ninyi watu hapa wa Jeffersonville. Mnamo mwaka wa 1933, ile Nuru ya kimbinguni ilishuka chini kule mtoni, siku ile nilipokuwa nikibatiza mia tano katika Jina la Yesu Kristo, kama yapata mvulana wa umri wa miaka ishirini. Ilisema nini, Jeffersonville? Ni kitu gani kilichokuwa chini ya Barabara ya Spring kule, wakati *Gazeti la Courier*, ninaamini lilikuwa ni *Louisville Herald*, lilichapisha makala Yake? Lilienda moja kwa moja kwenye Shirika la Wanahabari, moja kwa moja hadi Canada. Daktari Lee Vayle aliikata kutoka kwenye gazeti, huko juu huko Canada, mwaka wa 1933.

Nilipokuwa nikibatiza mtu wangu wa kumi na saba, chini ya Shahidi huyu; nawe unajua hadithi iliyosalia. Na wakati nilipokuwa nimesimama pale, nikibatiza mtu wa kumi na saba, Nuru ilishuka kutoka Mbinguni, ikiangaza juu juu pale, kama Nyota ikianguka kutoka Mbinguni. Sauti ilisema, "Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kuja kwa kwanza kwa Kristo, Ujumbe wako utatangulia Kuja Kwake kwa pili, ulimwenguni kote." Leo hii Maandiko haya yametimia.

44 [Kusanyiko linashangilia — Mh.] Siku hii! [Kusanyiko linashangilia sana na kumsifu Mungu.] Mungu aliahidi jambo hilo. Ni kitu gani kilichotukia? Leo hii imeenea kote ulimwenguni.

Na wakati Mungu aliposhuka kuja kule na kusema hilo, nilipokuwa mvulana mdogo, katika kijiti kilichowaka moto, ama kichaka kule juu, kikiwaka moto kwa Nguzo ya Moto, hapa juu mahali pa Wathen kule Utica Pike; nikiteka maji kule nyuma, kutoka kwenye kile kibanda hadi mahali pa kutengeneza pombe isiyo halali, mnajua ukweli wake. Yeye alisema, "Kamwe usivute sigara, wala kunywa pombe, wala kutia unajisi mwili wako, kwa kuwa kuna kazi ya kufanya utakapokuwa mtu mzima." Ninashuhudia kwamba hiyo ni Kweli, ya kwamba niliiona. Na Mungu, kama alivyofanya na Musa, alinena mbele ya kusanyiko kule, na kusema, "Hii ni Kweli."

Leo hii Maandiko haya yametimia katikati yetu.

Angalia yale aliyosema kuhusu upambanuzi, na jinsi utakavyokuwa; kutoka kuwawekea mikono, hadi kujua siri ya moyo. Leo hii Maandiko haya yametimia mbele ya macho yetu wenyewe.

45 Ahadi hizi zilizotolewa, angalia, ahadi hizi zote zilikuwa zimethibitishwa na kutimizwa na Mungu wa ahadi. Angalia, ikining'inia Washington, D.C., usiku wa leo, picha ya Malaika wa Bwana!

Kama vile George J. Lacy, mkuu wa alama ya kidole na waraka wa FBI kwa serikali ya Marekani, alilichunguza kutoka Houston, Texas, na kusema, "Hiki ndicho Kiumbe cha pekee cha kimbinguni kilichopata kupigwa picha ulimwenguni kote." Yeye alipaswa kujua; yeye ndiye aliye bora kuliko wote ulimwenguni, kwa hayo.

Angalia, hapo inaning'inia, kama Kweli, Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza Israeli kurudi kule nyikani. Unaongoza leo hii, Ujumbe wa aina ile ile, wa, "Kwea utoke Misri!" …?… Leo hii Maandiko haya yametimia. Mnajua Ujumbe aliosema.

46 Angalieni lile ono la Tucson, miaka mitatu iliyopita, wakati niliposimama hapa kwenye njia kuu. Wakati, miaka mitano kabla ya hapo, Yeye alisema, "Siku ile mji utakapopigilia kigingi mbele ya lango hilo, geukia upande wa Magharibi." Ninyi watu wa hekaluni ambao mmekuwa hapa, mnajua kuwa hilo ni sahi … wa-wakati huo. Hiyo ni kweli.

Na siku ile yule Bw.Goynes na hao wengine walikuwa kule juu, na kupigilia chini kile kigingi, nilimwambia mke wangu, "Kuna kitu fulani kuhusu jambo hili."

Akasema, "Ni kitu gani?"

Ndipo nikaingia na kuangalia katika kitabu changu kidogo. Ilikuwa hapo.

Na asubuhi hiyo iliyofuata, kwenye saa nne, nikiketi mle, chumba changu mle, yapata saa nne, Malaika wa Bwana akashuka. Akasema, "Nenda Tucson. Utakuwa kaskazini mashariki mwa Tucson, na watakuja Malaika saba katika kundi litakalotikisa dunia nzima inayokuzunguka." Kisha akasema, "Utaambiwa kutoka hapo."

Ni wangapi wanakumbuka jambo hilo, hapa, huko nyuma kabla halijatukia? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Kuna watu wanaoketi papa hapa katika jengo hili usiku wa leo, waliokuwa wamesimama papo hapo wakati jambo hilo lilipotukia.

Kisha akasema, "Ile Muhuri Saba ya siri zilizofichwa za Biblia nzima itafunguliwa, na kutimiza Ufunuo 10, ya kwamba katika Ujumbe wa Malaika wa saba mambo haya yatimie." Leo hii Maandiko haya yametimia mbele ya macho yetu. Leo hii Maandiko haya yametimia.

47 Mwaka jana, nikiwa nimesimama mahali pamoja, Bw. Woods hapa na mimi, tukipanda kilima, kwa namna fulani ya maombolezo, kuhusu mkewe kuwa mgonjwa. Roho Mtakatifu akasema, "Chukua jiwe lililowekwa pale. Tupeni hewani. Wakati itakaposhuka, semeni, 'BWANA ASEMA HIVI, kutakuwako na hukumu itakayopiga dunia.' Mwambie ya kwamba atauona mkono wa Mungu, saa chache zijazo."

Nikamwambia Bw Woods; yupo usiku wa leo. Na, nadhani, watu wanane ama kumi wa wale watu, ama kumi na watano, waliokuwako wakati huo ilipotukia; kesho yake asubuhi, ambapo Bwana alishuka katika upepo wa kisulisuli na kuurarua mlima ukituzunguka, na kukata vichwa vya miti, na kufanya milipuko mitatu, na kusema, "Hukumu inaelekea kwenye Pwani ya Magharibi."

Siku mbili baada ya hapo, Alaska karibu ilikuwa karibu kuzama chini ya dunia. Na tangu wakati huo, huku na huko Pwani, zinakokomoa hukumu ya Mungu dhidi ya kile kiambaza cha kiroho. Kuna pazia la chuma, kuna pazia la mianzi, na kuna pazia la dhambi.

48 Ustaarabu umesafiri pamoja na jua; vivyo hivyo na Injili. Wamekuja kutoka mashariki na kwenda magharibi, kama jua linavyokwenda. Na sasa iko kwenye Pwani ya Magharibi. Haiwezi kwenda mbele zaidi; kama ikienda mbali zaidi, itarudi mashariki tena.

Nabii alisema, "Kutatokea siku ambayo haiwezi kuitwa usiku wala mchana," siku ya kuhuzunisha, mvua nyingi na ukungu, ya kutosha tu haidhuru kujua jinsi ya kujiunga na kanisa au kuweka jina lako kitabuni. "Lakini itakuwa Nuru wakati wa jioni." Leo hii Maandiko haya yametimia.

J-u-a lile lile lipambazukalo mashariki ndilo j-u-a lile lile litualo magharibi. Na M-w-a-n-a wa Mungu yule yule aliyekuja mashariki na kujithibitisha Mwenyewe kama Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, ni M-w-a-n-a yule yule wa Mungu katika ulimwengu wa magharibi hapa, anayejitambulisha Mwenyewe miongoni mwa kanisa usiku wa leo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Nuru ya jioni ya Mwana imekuja. Leo hii Maandiko haya yametimizwa mbele zetu.

49 Tuko wapi katika wakati huu wa Ibrahimu? Tuko wapi katika wakati huu mkuu tunaosimama, saa kuu tunayoishi? Maono yote yametimizwa.

Vipi kuhusu wakati maskini mhudumu rafiki yetu hapa, kanisa dada mwenzangu, Junior Jackson, alipokuja mbio kwetu usiku mmoja, mimi kule chini. Kasema, "Nilikuwa na—na ndoto, Ndugu Branham, ambayo inanisumbua. Niliona ndugu wote wamekusanyika juu ya kilima." Kisha akasema, "Juu ya kilima hiki, mlikuwa mkitufundisha kutoka kwa herufi zilizoandikwa, ilionekana kama, katika herufi fulani ambazo wakati huo zilikuwa zimechongwa kwenye mwamba. Ulipomaliza jambo hilo, yote yaliyomalizika, ulituambia, ukasema, 'Njoni karibu,' nasi sote tukakusanyika."

Kasema, "Ulinyosha mkono kutokea mahali fulani na, ulionekana kama, ulichukua , kitu kama mtaimbo na kupiga kilele cha hiyo piramidi ndogo hata ikafunuka. Na, wakati ilipofunuka," kasema,"jiwe gumu lisili na maandishi juu yake. Nawe ulituambia 'tuangalie jambo hili.' Nanyi nyote … Sote tukaanza kuangalia." Kasema, "Nikageuza kichwa changu, nami nikawaona mkielekea magharibi, kwa nguvu sana mwezavyo, kuelekea machweo ya jua." Ni wangapi wanakumbuka jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

50 Nami nilisimama pale kidogo mpaka Roho Mtakatifu alipolifunua. Nilisema, "Biblia nzima, kadiri ilivyofunuliwa kwa mwanadamu, kwa kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, ubatizo katika Jina la Yesu, na mambo haya yote, yamefunuliwa; bali kuna siri zilizofichwa ndani, kwa sababu Biblia imetiwa muhuri kwa Mihuri Saba. Sina budi kwenda kule kuipata."

Asubuhi hiyo wakati wale Malaika saba waliposhuka na kuiharibu dunia, na miamba iliruka kila upande, Malaika saba walisimama pale na kusema, "Rudini Jeffersonville, kule mlikotoka, kwa maana zile Muhuri Saba za zile siri saba zitafunguliwa."

Tuko hapa, leo, tukifahamu *Uzao wa Nyoka.* Katika siku chache, Mungu akipenda, tutaelewa usahihi wa *Ndoa na Talaka.* Na mambo haya yote ambayo Mungu ameyafungua, kila Muhuri, zile siri tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Nasi tumekuwa katika furaha, Uwepo wa baraka Zake! Hiyo ni kweli. Siku hii, Andiko hili!

51 Lile gazeti liitwalo Life liliandika habari juu yake, "Duara ya siri ya nuru inakwenda juu hewani juu ya Tucson na Phoenix," katika njia ile ile niliyowaambia yapata mwaka moja kabla haijatendeka, jinsi ingekuwa, na kama umbo lenye pembe tatu. Picha hiyo inaning'inia kanisani kule chini. Wewe uliyechukua

gazeti hilo unalo. Hilo hapo, kabisa. Wakasema, "Ni maili ishirini na saba kwenda juu na maili thelathini kwenda juu." Wao bado hawaelewi kilichotukia. Ilionekana kisiri na ikaenda kisiri.

Ndugu Fred Sothmann, mimi na Ndugu Gene Norman, tukisimama pale. Mashahidi wa tatu. Kama vile alivyopanda juu ya mlima; Petro, Yakobo, na Yohana, kutoa ushuhuda. Nilisimama pale na kuangalia jambo hilo lilipotukia, na kuona likitendeka.

Hiyo hapo, ikining'inia angani; kufikia sasa, hakuna unyevu, hakuna unyevu wala cho chote cha kufanya m—ukungu. Lingekuwaje kule? Walikuwa ni Malaika wa Mungu wakirudi, baada ya Ujumbe wao. Leo hii unabii huo umetimia miongoni mwetu. Leo hii Maandiko haya yametimia.

Angalia, Mihuri Saba imefunguliwa. Upepo wa kisulisuli kuelekea Pwani ya Magharibi. Sasa, msilikose, kama walivyofanya huko nyuma.

52 Sasa, usikivu wetu, uko karibu kidogo na siku zetu. Maandiko yanasema nini kuhusu siku hizi, na kuhusu wakati tunaoishi? Yesu akinena … Sitakuwa na wakati wa kuyachukua yote, bali ninataka kuchukua hili kabla hatujafunga.

Yesu alisema, katika Luka Mtakatifu mlango wa 17, kifungu cha 30. Yesu Kristo, Neno Mwenyewe! Unaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Yesu Kristo, Neno Mwenyewe, aliyefanyika mwili, alinena na kusema kile Neno lingekuwa katika wakati wa mwisho, itakuwaje ishara ya mwisho wa ulimwengu. Yeye aliwaambia taifa lingeinuka dhidi ya taifa, bali Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika siku atakapofunuliwa Mwana wa Adamu."

Sasa, wakati Yesu alipokuja duniani, Yeye alikuja katika jina la Wana watatu. Mwana wa Adamu, ambaye ni nabii; Mwana wa Mungu; na Mwana wa Daudi.

Sasa, Yeye aliishi hapa duniani. Yeye hakusema kamwe alikuwa Mwana wa Mungu. Yeye alisema, "Mimi ni Mwana wa Adamu." Yehova Mwenyewe aliwaita Ezekieli na manabii, "Mwana wa Adamu." Kwa sababu, ilimbidi kuja kutimiza Maandiko kama nabii. Musa alisema, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama mimi." Hiyo ndiyo sababu asingeweza kuwa Mwana wa Mungu pale, kwa sababu alikuwa Mwana wa Adamu. Yeye … "Neno liliwajia manabii." Naye alikuwa Neno katika utimilifu Wake. Mwana wa Adamu, yule—yule nabii mkuu … Si nabii mkuu, bali Mungu-Nabii, "Utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili ulikuwa ndani Yake." Kwa hiyo, Yeye alikuwa ni Mwana wa Adamu.

Sasa, kwa miaka elfu mbili, Yeye amejulikana kwetu kama Mwana wa Mungu, Roho.

Na katika ule Utawala wa Miaka Elfu, Yeye atakuwa Mwana wa Daudi, juu ya kile Kiti cha Enzi. Sote tunajua jambo hilo, mnaoamini Maandiko.

53 Sasa, Yesu alisema, mwishoni tu mwa wakati huu wa kanisa tunaoishi, ya kwamba, "Mwana wa Adamu angefunuliwa tena kwa jinsi ile ile ilivyokuwa, kama ilivyokuwa Sodoma."

Angalia vile, Yeye alivyoitoa, kihistoria. Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku hizo," kwanza, "za Nuhu, jinsi walivyokuwa wakila, wakinywa, wakioa, na kuolewa." Ndipo Yeye akataja, ya pili, kutoka mwisho juu ya Mwana wa Adamu katika Sodoma. Maana, hapo Yeye alikuwa akiwashughulikia Wayahudi; hapa, huko Sodoma, Yeye anashughulika na Mataifa. Hapo, Yeye aliwazamisha wote kwa maji, katika hukumu; hapa, kwa Mataifa, Yeye aliwateketeza wote katika siku ya Sodoma. Hiyo ni kweli. Ulimwengu wa Mataifa uliwaka pale, "na ndivyo itakavyokuwa wakati Mwana wa Adamu atakapofunua." Si maji tena, bali itakuwa moto wakati huu. Yesu alisoma Mwanzo 23 tunayoisoma, Yeye aliposoma kuhusu Sodoma.

54 Sasa, tunakubali hali ambayo imenenwa, juu ya hali ya ulimwengu ya Sodoma, Usodoma, hali ya Sodoma. Sisi, kila mmoja, tutasema "amina" kwa hilo. Tunaamini jambo hilo. Vema.

Na hali ya kiroho ya Laodikia, kanisa la kawaida, tutasema "amina" kwa hilo, na kuzikubali ishara zao. Tunajua ya kwamba kila ishara ipo. Kanisa liko katika Laodikia. Tunajua jambo hilo. [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Tunajua ulimwengu uko katika hali ya Sodoma. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Tutakubali jambo hilo.

Lakini vipi kuhusu ishara ya Ibrahimu, yule anayemngojea mwana aliyeahidiwa? Hiyo ilikuwa ni nyingine.

Kumbukeni, walikuwa na Sodoma kule nyuma; walikuwa na mjumbe wao. Naye Ibrahimu alikuwa na Mjumbe kwake.

Ibrahimu alikuwa akingojea, siku baada ya siku, karibu, jambo lisilowezekana kutukia. "Sara, tisini, naye mia." Kulingana na ahadi ya Mungu, alikuwa angali anangojea. Katikati ya ukosoaji wote, alikuwa akimngojea mwana huyo.

Vivyo hivyo na mwamini wa kweli angali anamngojea yule Mwana aliyeahidiwa kurudi! Angalia, kabla tu ya mwana kuwasili, alipewa ishara. Je! Si ishara ya Mwana ajaye kufunuliwa kwa Uzao wa kifalme wa Ibrahimu anayemngojea Mwana wa Kifalme, kama vile ilivyokuwa kwa baba Ibrahimu kwa ajili ya mwana wa kawaida? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Hiyo ni kweli? ["Amina."] Yesu alisema hivyo, hapa katika Luka Mtakatifu 17:30, "Kabla ya wakati huu kuja, ya kwamba, Mwana wa Adamu atafunuliwa kama alivyofanya katika siku za Sodoma, kabla ya maangamizi ya Sodoma." Sasa tunatafuta ishara.

55 Sasa hebu na tuchukue hali ya wakati kama ilivyokuwa Sodoma. Angalia, wote walitoka kwenda Sodoma, ulimwengu.

Nafikiri mmoja wa waongozaji wa sinema aliweka picha, si muda mrefu uliopita, nami ilinibidi kuiona, hiyo ilikuwa, *Sodoma*. Kama ukipata kuona jambo hilo na hakuna kitu kingine ila hilo, liangalie. Hakika ni picha nzuri ya Marekani leo, Hollywood, hasa kabisa; mavazi ya aina ile ile na kila kitu kingine walichofanya wakati huo; michezo ya ulevi wa kupindukia na kila kitu kinginecho, kundi la watu wa kidini lililojitenga, linalojiita la kidini.

Angalia, na Sodoma ilikuwa na shahidi, na ilikuwa ni jamaa mmoja jina lake Lutu, ambaye alikuwa mpwa tu kwa—kwa Ibrahimu.

Sasa, Ibrahimu hakushuka kwenda Sodoma, yeye na kundi lake. Alikuwa na kundi kubwa pamoja naye, la kutosha kupigana kama na wafalme dazani moja na jeshi lao. Kwa hiyo, alikuwa na kundi kubwa pamoja naye. Naye alikuwa ameketi huko nje chini ya mwaloni, siku moja, wakati kila kitu kilikuwa kimemwendea vibaya; hakuna mtu aliyekuwa na uhusiano wowote naye, bali alikuwa bado ameshikilia ahadi hiyo.

Angalia sasa, kwa makini, kabla hatujafunga.

Wakati alipokuwa ameketi pale, wakaja watu watatu, wakimwendea. Wawili wao walishuka wakaenda Sodoma na kuwahubiri Injili, wapate kutoka, kwa Lutu. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Lakini Mmoja alikaa na Ibrahimu. Angalia, Yule aliyekaa na Ibrahimu alikuwa ni Mungu Mwenyewe. Hao wengine wawili walikuwa ni wajumbe wa Malaika.

56 Sasa, huko chini Sodoma, hawakufanya miujiza, ila kuwapiga tu upofu. Na kuhubiri Injili daima huwapofusha.

Sasa angalia mpangilio wa siku hiyo. Kuna kanisa la kawaida. Daima katika tatu, kama nilivyosema jana usiku, Mungu anawakilishwa. Kulikuwako na Wasodoma; Waloti; na wa Ibrahimu. Liko mahali pale pale usiku wa leo, ulimwengu ukiwa hivyo tu.

Hebu niwaulize jambo fulani. Angalia mazingira haya sasa. Ibrahimu alimwita Mtu huyu aliyezungumza naye, "Elohimu." Neno la Kiebrania Elohim linamaanisha "Yeye ajitoshelezaye kwa yote, Yeye aliye wa Milele," Elohimu, Mungu Mwenyewe!

Hapo mwanzo, Mwanzo 1, ilisema, "Hapo mwanzo Mungu …" Chukua neno la Kiebrania pale, ama, ama neno la Kiyunani, hasa, "Hapo mwanzo Elohimu aliumba mbingu na nchi."

57 Hapa, Yeye, katika Mwanzo, yapata 22 hapa, Yeye anasema tena, ama—ama kama wale 20, Yeye alisema, naye akaliita jina la Mtu huyu "Elohimu." Kwa nini alifanya hivyo? Mungu, aliyewakilishwa katika mwili wa kibinadamu, aliyeketi pamoja na Ibrahimu na kula sandwichi ya ndama, akinywa maziwa, na kula mkate. Mungu Mwenyewe, na akatoweka moja kwa moja mbele za Ibrahimu.

Lakini Yeye alimpa ishara. Angalia. Na ishara hiyo ilikuwa ni kwamba alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema.

Na kumbuka Ibrahimu jina lake lilikuwa Abramu siku chache hapo kabla, na Sara alikuwa Sarai hapo kabla—S-a-r-a-i, ndipo S-a-r-a na A-b-r-a-m-u kuwa I-b-r-a-h-i-m-u. Ibrahimu maana yake ni "baba wa mataifa."

Sasa angalia kwa makini sana hapa, nasi tutaona mandhari ya saa tunayoishi sasa, kama Yesu alivyotuambia tutazame mazingira haya. Tumeona mengine yote sawa; sasa hebu na tuone Mzao wa kifalme, ni mazingira gani wanayopaswa kuona.

Sasa Mtu huyu alisema, "Ibrahimu, yu wapi mkeo, Sara?"

Naye Ibrahimu akasema, "Yumo hemani, nyuma Yako."

Sasa, Yeye hakuwa amemwona. Yeye alijuaje ya kwamba jina lake lilikuwa Ibrahimu? Yeye alijuaje jina lake lilikuwa S-a-r-a-h? "Ibrahimu, yu wapi mkeo, Sara?"

Kasema, "Yumo hemani, nyuma Yako."

Yeye alisema, "Mimi …" "Mimi," kiwakilishi nafsi. "Nitawazuru kulingana na ahadi. Mke wako atampata mtoto huyo. Mmenitumaini, sasa nitalifanya litimie."

58 Naye Sara, akiwa hemani, nyuma, akidukiza ama kudoya, cho chote mkiitacho, akisikiliza akiwa hema, akacheka kimoyomoyo, na kusema, "Sasa, mimi, mwanamke mkongwe kama nilivyo mimi, niwe na raha na bwana wangu; na yeye akiwa mzee, pia, zaidi ya umri wa miaka mia moja? Wakati, hili halijatukia kwa miaka mingi, mingi sana."

Na yule Mtu, M-a-n, ameketi pale akila, katika mwili wa kibinadamu, akinywa na kula kama mtu wa kawaida; akiwa na mavumbi kwenye nguo Zake, na alikuwa na mavumbi miguuni Mwake, naye Ibrahimu akayaosha. Mungu, Mwenyewe, aliangalia kila mahali, Naye akasema, "Kwa nini Sara akacheka, huko hemani, akisema jambo *hili?"* Alijua, angeweza kutambua mawazo ya Sara hemani, nyuma Yake. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Sasa, wakati Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu ulipokuja duniani, Yeye alionyesha ishara gani, Mwana wa Adamu. Simoni alimjia siku moja; Andrea alimleta. Yeye alisema, "Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona,"Yeye alisema. Mnaona, hilo lilimfanya awe mwamini kutoka naye.

59 Filipo akaenda kule akamleta Nathanaeli; akarudi, kasema, "Njoo, umwone Mtu ambaye tume—tumempata; Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu."

Akasema, "Sasa ngoja kidogo. Kuna kitu kizuri kinachoweza kutoka kwenye ushupavu huo wa dini?"

Akasema, "Njoo, uone."

Kwa hiyo wakati Filipo alipokuja katika Uwepo wa Yesu, pamoja na Nathanaeli, Yesu alimwangalia na kusema, "Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake."

Akasema, "Rabi, ulinijua lini?"

Kasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona."

Yeye alisema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli!"

60 Wakati maskini yule mwanamke kisimani, katika hali yake ya uzinzi, alipokuja, kitu kidogo kama hiki, kuteka maji. Yesu alikuwa amewatuma wanafunzi Wake waende, wapate chakula. Wakati alipokuja kuteka maji, Yeye alisema, "Nipe maji ninywe, ewe mwanamke."

Akasema, "Si desturi Kwenu kusema hivyo. Tuna ubaguzi hapa. Sasa, ninyi Wayahudi hamna uhusiano wowote nasi Wasamaria; hatuna uhusiano wowote nanyi."

Yeye alisema, "Lakini, ewe mwanamke, kama ungalijua ni Nani unayezungumza naye, ungeniomba Mimi maji. Nitakupa maji usije ukayateka hapa tena."

Yeye alipata hali yake ilivyokuwa, namna ilivyokuwa. Akasema, "Nenda kamlete mumeo uje naye hapa."

Akasema, "Sina mume yeyote."

Yeye alisema, "Umesema kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa si wako."

Akasema, "Bwana, naona ya kwamba Wewe ni nabii. Tunajua Masihi ajapo Yeye atatuonyesha mambo haya."

Yesu alisema, "Mimi Ndiye."

Juu ya jambo hilo, alikimbilia mjini na kusema, "Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo niliyofanya. Je! Huyu si ndiye Masihi hasa?"

61 Angalia, Yeye alifanya jambo hilo mbele ya Wayahudi, na Wasamaria, bali si Mataifa. Mataifa, sisi watu, tulikuwa makafiri katika siku hizo, mataifa mengine, wakibeba rungu mgongoni mwetu, tukiabudu sanamu. Hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote.

Yeye huonekana tu kwa wale wanaomtazamia, nasi tunapaswa kuwa tunamtarajia.

Lakini wale waliodai wanamtafuta, kanisa lenyewe, walipoona hilo likitendeka, walisema, "Yeye ni pepo. Yeye ni mpiga ramli, Beelzebuli!"

Naye Yesu alisema, "Watasamehewa dhambi hiyo," kwa sababu Yeye alikuwa hajafa bado. "Lakini," kasema, "siku moja Roho Mtakatifu atakuja na kufanya jambo lile lile, na kunena neno moja dhidi Yake kamwe hakutasamehewa." Hiyo ni siku hii, ambapo kila Neno halina budi kushikamana pamoja. "Nena neno dhidi Yake; kamwe haitasamehewa katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao."

62 Huo ulikuwa Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu. Na hapa yule Mzao wa Kifalme wa Ibrahimu, ambaye alikuja kwa sababu ya utambulisho wa Mtu yule aliyeketi pale pamoja na Ibrahimu, alikuja kuthibitisha ilikuwa ni Mungu yule yule, akiahidi katika siku hii, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu, wakati anapojifunua kama Mwana wa Adamu." Amina. Hii ndiyo siku ya Andiko hili kutimizwa.

Angalia mahali tulipo leo. Angalia kanisa ambapo Mwana wa Mungu … Angalia siku ya huzuni. Angalia unabii wote. Sasa, jambo la ajabu, wageni wetu wanastahili wakati huo, kama mazingira hayana budi kuwa kama kule Sodoma.

Kulikuwako na watatu wao waliokuja, watu watatu mashuhuri waliotumwa kutoka Mbinguni. Tutakubali jambo hilo. Watatu wao; Mmoja alikaa na Ibrahimu. Wote walianzia pale, bali Mmoja alikaa na Ibrahimu. Hao wengine walishuka wakaenda Sodoma. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Na Ibrahimu alikuwa na jina lililobadilishwa, kutoka Abramu likawa Ibrahimu. Kweli? ["Amina."]

Hakuna hata wakati mmoja ambapo historia, kanisa la ulimwengu, limewahi kuwa na mwinjilisti wa kuliendea, lenye jina linaloishia katika h-a-m, mpaka leo hii, Billy G-r-a-h-a-m. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] G-r-a-h-a-m, herufi sita. A-b-r-a-h-a-m ni herufi saba. Lakini G-r-a-h-a-m ni herufi sita, ambazo ni ulimwengu, mwanadamu. Mnaona?

63 Angalia kilichotoka kule, leo, ni hao wajumbe kutoka Mbinguni.

Kuna mtu duniani aliye na toba iliyohubiriwa waziwazi sana kama Billy Graham? Kuna mtu ambaye amekuwa na ushawishi kwa watu, kama Billy Graham? Kamwe hapajakuwako na mtu, kimataifa. Loo, Billy Sunday, na kadhalika, alikuwa hapa Marekani, lakini Billy Graham anajulikana kote ulimwenguni. Mnaona mahali anaitia? Kutoka Sodoma.

Naye ana kundi lake limeshirikishwa pale pamoja na kanisa la Kipentekoste, Oral Roberts.

Lakini vipi kuhusu kundi la Wateule? Wanapaswa kuona ishara ya namna gani? Wanapaswa kuwa na nini? Haleluya! "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Leo hii Maandiko haya yametimia. [Kusanyiko linafurahi — Mh.] Siku hii ahadi ya Mungu imetimia. Tunajua jambo hilo kuwa ni Kweli. Yeye yuko hapa usiku wa leo kama alivyokuwa wakati huo.

64 Sasa, kuhubiri jambo hilo, ambalo nilisema muda mfupi uliopita, kama ukihubiri chochote na ni Kweli ya Injili, basi Mungu anawajibika kuthibitisha hilo. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Sasa, kama hivyo ndivyo ilivyo, hebu Mungu aliyeandika Neno, hebu Mungu aliyetoa unabii, hebu Mungu ambaye ni Mungu wa Neno, aje na kuthibitisha ya kwamba Yeye angali ni Mungu.

Wakati Eliya alipopanda mlimani; akiangalia, Elisha akaenda akimwangalia Eliya, akasema, "Ninataka sehemu maradufu." Na vazi lililokuwa juu ya Eliya likamwangukia Elisha. Alitembea chini, na kuinua ile blanketi maradufu na kuupiga mto, na kusema, "Yuko wapi Mungu wa Eliya?" Na jambo lile lile lililotukia kwa Eliya, lilitukia kwa Elisha.

Na Injili ile ile, Nguvu zile zile, Mwana wa Adamu yule yule aliyekuwako jana, yupo leo, na atakuwa milele. Waebrania 13:8. Mnaamini jambo Hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Halafu, nawauliza. Siwezi kuwa Yeye, bali Yeye yuko hapa. ["Amina."] Sisi ni mbebaji tu.

65 Baadhi yenu ninyi watu huko nje, ambao ni wagonjwa na wanaoteseka, ambao mnajua ya kwamba siwajui, hebu Mungu sasa … kama ninaweza kujinyenyekeza vya kutosha. Unaomba na kumsihi Mungu.

Sidhani … Hakuna kadi ya maombi humu jengoni, sivyo? La, mimi si … Kamwe hatutumii kadi zozote za maombi. Tutafanya mkutano wa maombi kwenye … ama uponyaji wa wagonjwa, kanisani. Lakini, ombeni.

Nanyi mnajua ya kwamba mimi si mgeni kwenu kabisa. Mnaona, mnanijua mimi, Jeffersonville! Sitaki watu kutoka Jeffersonville wafanye hivyo. Ninataka watu kutoka mbali mahali hapa. Angalia kama Mungu bado hufunua! Angalia kama Yeye angali ni yeye yule jana, leo, na hata milele!

Fanya kama yule maskini mwanamke huyo alivyofanya. Akapita, naye akasema, "Namwamini Mtu huyu." Alikuwa akitokwa na damu, naye akasema, "Kama ninaweza kugusa upindo wa vazi Lake, ninaamini nitapona." Hiyo ni kweli?

Kwa sababu ya imani yake, siku hiyo, Maandiko yalitimia. "Anaufunga moyo wa waliovunjika moyo, akawaponya wagonjwa na vilema."

Wakati alipoligusa vazi Lake, na akatoka akaenda na kuketi chini, Yeye aligeuka na kusema, "Ni nani aliyenigusa?" Yeye alijuaje, katika umati huo mkubwa wa watu, labda mara thelathini walio hapa usiku wa leo, maelfu yao? Yeye alijuaje jambo hilo? Yeye alisema, "Ni nani aliyenigusa?" Yeye hakusema hilo kwa kusema tu; Yeye alisema hivyo kwa sababu ilikuwa ni kweli. Naye akasema, "Ni nani aliyenigusa?" Na moja kwa moja akaangalia kote na kumwona maskini mwanamke huyo, mahali alipokuwa ameketi ama

amesimama, mahali po pote alipokuwa, akamwambia kutokwa kwake na damu kumekwisha.

Huyo alikuwa ni Yesu jana. Huyo ni Yeye leo. Unaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

66 Sikujui; Mungu hufanya hivyo. Bali una maumivu ubavuni mwako, hilo linakusumbua. Hiyo ni kweli. Umeketi pale ukiomba juu ya jambo hilo. Je! Mimi ni mgeni kwenu, nasi hatufahamiani? Simama, kama ndivyo ilivyo. Sikujui. Ni mtu *huyu* papa hapa pembeni, jamaa huyu kijana. Pia una koo baya. Hiyo ni kweli. Unaomba juu ya jambo hilo. Nyote mna wasiwasi kuhusu jambo fulani. Itawabidi kuondoka mkutanoni kwa sababu, wewe ni mhudumu, una ahadi fulani unazopaswa kushughulikia. Hiyo ni kweli. A-ha. Unaamini Mungu anakujua wewe ni nani? Mchungaji Bw. Smith, sasa unaweza kwenda na kuponywa. Yesu Kristo alikufanya mzima. Nenda kwenye mkutano wako; koo lako halitakusumbua.

Alimgusa nani?

67 Kuna mtu anayeketi papa hapa nyuma; anateseka. Ana uvimbe kwenye mapafu yake ya kushoto. Yeye haninii … Yeye hatoki hapa. Umekuwa mfanyakazi wa mgodi. Hiyo ni kweli. Mimi ni mgeni kabisa kwenu. Kama hiyo ni kweli, peana mkono. Uvimbe huo uko kwenye mapafu yako ya kushoto, nawe uko tayari kufanyiwa upasuaji mara moja. Hiyo ni kweli? Wewe hutoki hapa. Umetoka nje ya mji. Umetoka Virginia. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anakujua wewe ni nani? Bw.Mitchell, hiyo ni kweli, nenda nyumbani ukapate afya. Yesu Kristo anakufanya mzima. Mwulize huyo mtu! Sijapata kumwona, maishani mwangu. Alikuwa ameketi pale, akiomba.

Leo hii Andiko hili!

[Ndugu Branham anageuka na kulipa kisogo kusanyiko — Mh.] Huyu hapa mama anayeketi papa hapa nyuma, nyuma yangu, kama Sara alivyokuwa hemani. Yeye anamwombea binti. Simama. Binti hayupo hapa; yuko mbali, binti. Nawe ni kama vile ilivyokuwa wakati mwanamke alipomjia Yesu, ambaye alikuwa na mwanamke aliyekuwa amesumbuliwa na mapepo mbalimbali. Mwanamke ni … msichana ana pepo. Yeye hayupo hapa. Ametoka … Umetoka Carolina ya Kaskazini. Unaamini jambo hilo? Na hiyo ni kweli, sivyo? Bibi Orders, unaweza kwenda nyumbani. Ukiamini kwa moyo wako wote, utamkuta binti yako kama yule alivyokutwa zamani za Yesu Kristo katika siku zilizopita; kasema aliponywa.

68 Leo hii Maandiko haya; ile ishara ya Sodoma, ishara ya ule Mzao mkuu, ishara ya kanisa la kawaida! Leo hii Maandiko haya yametimizwa miongoni mwenu. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Utamkubali sasa hivi kama Mwokozi na mponyaji wako? Simama kwa miguu yako, kila mmoja wenu, useme, "Ninakubali uponyaji wangu. Ninamkubali kama Mwokozi wangu. Ninamkubali kama Mfalme wangu." Kila mmoja simameni kwa miguu yenu.

Siku hii! Sikilizeni, enyi marafiki.

"Yeye alisoma Maandiko, akamrudishia kuhani Biblia, na," kasema, "macho yote ya watu yalikuwa yamemkazia macho. Naye akawaangalia, na kusema, 'Leo Maandiko haya yametimia.'"

Nimesoma Maandiko, pamoja na dhihirisho dazani moja au zaidi ya kwamba tunaishi katika siku ya mwisho, kizazi kitakachomwona Yesu Kristo akirudi duniani. Nami nawaambia usiku wa leo, tena, leo Maandiko haya yametimizwa mbele zenu.

Ninyi huko Tucson, ninyi huko California, ninyi huko New York, kwenye mawasiliano haya ya simu, leo Maandiko haya yametimizwa mbele zenu.

Na tufurahi na kushangilia, kwa maana Arusi ya Mwana-Kondoo imekaribia, na Bibi-arusi Wake … Bibi-arusi Wake amejiweka tayari.

Hebu na tuinue mikono yetu na kumpa utukufu, enyi watu wote. Mungu akubariki. [Kusanyiko linaendelea kushangilia na kumsifu Mungu — Mh.]

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7